

KATIKA MAHKAMA KUU ZANZIBAR

IMESIKILIZWA VUGA

KESI YA MADAI RUFAA NAM. 7 YA 2013 MAHKAMA KUU

KUTOKA RUFAA YA MADAI NAM. 46/2012 MAHKAMA YA KADHI WA RUFAA VUGA

KUTOKANA NA KESI YA MADAI NO. 464/2012 MAHKAMA YA WILAYA

MWANAKWEREKWE

KHALID KASSIM HAJI

.....

MUOMBA RUFAA

DHIDI YA

MWANAKOMBO KHATIB SAID

.....

MPINGA RUFAA

H U K U M U

Omar Makungu, Jaji Mkuu.

Muomba rufaa Bw. Khalid Kassim Haji amewasilisha rufaa hii baada ya kuwa hakuridhika na maamuzi pamoja na hukumu iliyotolewa na Mhe. Kadhi Mkuu Shk. Khamis Haji Khamis tarehe 16/1/2013. Hukumu hiyo inayolalamikiwa na Muomba rufaa imemtaka Mpinga rufaa (mke) kujikhuluu katika ndoa yake kwa kurejesha nusu ya mahari na kutengua ndoa na kupewa talaka yake. Kutokana na hukumu hiyo Muomba rufaa amewasilisha sababu zake 3 za rufaa kama ifuatavyo:-

1. Kwamba Mhe. Kadhi Mkuu hakuzingatia katika maamuzi yake kwa kumtaka Muomba rufaa (mume) kurejeshewa nusu ya mahari (Tshs.

395,000/=) na Uamuzi wa kutengua ndoa na kupewa talaka Mpinga rufaa (mke).

2. Kwamba; Mhe Kadhi Mkuu alipitikiwa kisheria kwa kumtaka Mpinga rufaa kurejesha nusu ya mahari na kutengua ndoa na kupewa talaka (Mpinga rufaa) kutokana na uzito wa ndoa sababu mimi mume Muomba rufaa sikushindwa kumtafutia sehemu ya kumuweka mke (Mpinga rufaa).
3. Kwamba; Kwa kutokuwa na sababu nzito za kisheria za kusimamisha talaka.

Muomba rufaa ameiomba Mahkama hii itengue maamuzi yaliyotolewa na Mahkama ya Kadhi wa rufaa yaani Kadhi Mkuu.

Wakati wa kusikiliza rufaa Muomba rufaa alieleza Mahkamani kuwa kutokana na hali ya mgogoro ulivyo haukuwa na uzito wa kuvunja ndoa. Matatizo yaliyotokea ni ya kibinaadam na yasichukuliwe kuwa ni kikwazo kwani yanaweza kusawazishwa. Hivyo ameomba Mahkama kuzipa uzito sababu zake za rufaa na kuzikubali.

Kwa upande wake Mpinga rufaa amepinga rufaa hii kwa sababu ameona haina uzito. Alieleza kuwa hukumu iliyotolewa na Kadhi Mkuu ni sahihi na anaikubali. Alieleza kuwa sababu zilizotolewa na Muomba rufaa hazina msingi

na yeye hayuko tayari kurejea kwa Muomba rufaa kutokana na udanganyifu alioufanya kabla ya ndoa yao na ndani ya ndoa yao hata kupelekea kuomba talaka Mahkamani. Ameomba rufaa ikataliwe.

Mahkama baada ya kusikiliza hoja za pande zote mbili na baada ya kupitia kwa uangalifu mwenendo wa kesi hii tokea katika Mahkama ya Kadhi wa Wilaya – Mwanakwerekwe imeona kuwa Muomba rufaa ametumia khadaa kubwa katika ndoa hiyo. Muomba rufaa ameanza khadaa kabla ya ndoa, ndani ya ndoa na hata Mahkamani amejaribu kusema uongo. Katika hukumu yake Kadhi wa Wilaya alimtaka Mpinga rufaa (mke) arudi kwa mume (Muomba rufaa) kwa masharti yafuatayo:-

1. Muomba rufaa awatake radhi wazazi wa Mpinga rufaa juu ya maneno aliyoyasema.
2. Muomba rufaa (Mdaiwa) atoe shilingi laki moja ampe mke wake kama ni fidia kwa maneno aliyomwambia pia apate kununua nguo kwani ilikuwa bado hajamnunulia.
3. Mdaiwa (Muomba rufaa) amtafutie nyumba mdai (Mpinga rufaa) ya kukaa iwe na choo na jiko.
4. Mdaiwa (Muomba rufaa) ayafanye haya kabla ya mdai hajaenda kwa Mdaiwa.

5. Mdaiwa (Muomba rufaa) anapewa muda wa miezi mitatu awe ameshatekeleza hayo yote.
6. Ikimalizika siku alizopewa yaani miezi mitatu bado hajatekeleza basi mdai (Mpinga rufaa) itapasa aje achukue talaka yake.
7. Na mwisho mdaiwa (Muomba rufaa) iwapo ameyatekeleza masharti yote, itamlazimu amhudumie mdai (Mpinga rufaa) kwa chakula, nguo na matumizi. Masharti haya yametolewa na Mahkama ya Kadhi wa Wilaya tarehe 10/9/2012.

Baada ya kuwasikiliza kwa makini Muomba rufaa na Mpinga rufaa, Mahkama hii inamaoni kuwa Muomba rufaa ameshindwa kutekeleza masharti yaliyotolewa na Mahkama ya Wilaya na hivyo kutoa mwanya kwa Mpinga rufaa kupewa talaka yake. Imebainika kuwa Muomba rufaa ni mdanganyifu sana na hajawa tayari kuwa na mke kwa wakati huu kwa kuwa ameshindwa kutekeleza mambo ya lazima katika ndoa nayo ni makazi, chakula na mavazi. Kutokana na hali hiyo Mahkama hii inaikataa rufaa hii.

Mahkama hii inaamua kama ifuatavyo:-

1. Hukumu ya Kadhi Mkuu ya tarehe 16/1/2013 inafutwa.

2. Mpinga rufaa apewe talaka yake na Mahkama kwa kufasikhi ndoa.
(fasikh).
3. Kila upande utabeba gharama zake za kesi hii. Hii ndio hukumu ya Mahakama hii.

Sgd: Omar O. Makungu - CJ

30/5/2013

1. Sgd: Shk. Uwesu Machano
2. Sgd: Shk. Juma Fakih
3. Sgd: Shk. Kani Mkanga
4. Sgd: Shk. Fadhil P. Pandu

Hukumu hii imetolewa leo tarehe 30/5/2013 mbele ya Mpinga rufaa na Muomba rufaa akiwa hayupo.

Sgd: Omar O. Makungu – CJ.

30/5/2013

Nathibitisha kuwa hii ni nakala sahihi ya hati ya asili.

Sgd. George J. Kazi

MRAJIS,

MAHKAMA KUU - ZANZIBAR

